

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA TANO

09 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA TANO – TAREHE 09 APRILI, 2026

I. DUA:

**II. KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDU
KWA WABUNGE:**

1. Mhe. Angela Charles Kizigha
2. Mhe. Dkt. Evaline Wilbard Munisi

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**36. MHESHIMIWA JASMINE CHESCO NG'UMBI (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Vijana wanapata ajira katika Miradi mikubwa kama SGR na Viwanja vya Ndege.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

37. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (CHAMAZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara katika eneo la Kwa Mwarabu Kata ya Kilungule ili kuondoa adha ya usafiri kwa Wananchi.

38. MHESHIMIWA AMINA MUSSA MKUMBA (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Stendi Kuu ya Mabasi Kibiti.

39. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Miundombinu ya Shule ya Sekondari Mashimba katika Halmashauri ya Maswa.

40. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua kiwango cha Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mkoa wa Mara.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

41. MHESHIMIWA DKT. NEEMA PETER MAJULE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusajili Wawekezaji wote nchini kupitia TISEZA ili kuwa na kanzidata sahihi ya Wawekezaji.

WIZARA YA KILIMO:

42. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Maghala Baridi mawili ya kuhifadhia zao la Parachichi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

43. MHESHIMIWA MARIRTA GIDO KIVUNGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa huduma ya Dawa na Chanjo muhimu ili kuboresha afya na kuongeza thamani ya Mifugo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

44. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka gari la Zimamoto katika Wilaya ya Mbulu.

WIZARA YA MAJI:

45. MHESHIMIWA CHARLES JACOB SUNGURA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka Maji Safi na Salama kutoka Mto Wami katika Mji wa Mkata.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
09 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**